
# Katiba ni nini?

## Katiba na haki



Kitabu hiki kimetolewa na **Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)** ikishirikiana na **Twaweza.**

**Waandishi:** Anna Henga, Evarist Kamwaga na Al-Amin Kheraj

**Wahariri:** Helen Kijo - Bisimba, Rakesh Rajani na Risha Chande

**Mchoraji:** Marco Tibasima

**Anuani:**

SLP 75254, Dar es Salaam.
Simu: 2773048/ 2773038
Nukushi: 2773037
Barua pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakili na kutuma nakala mbili kwa LHRC.

# Utangulizi

Msomaji,

Wengi tumekua tukisoma au kusikia Katiba. Zaidi ya hayo, wengi tukadhani neno au dhana hii haituhusu bali ni maalumu kwa wanasheria au wasomi tu. Ukweli ni kwamba, Katiba ni kitu muhimu mno. Kama msingi ulivyo na umuhimu katika ujenzi wa nyumba, kadhalika na Katiba ni muhimu sana kwa Taifa na watu wake. Pia ina uhusiano wa moja kwa moja na maisha yetu ya kila siku.

Kijitabu hiki kitakuwezesha kutambua maana na umuhimu  wa Katiba yaani jinsi inavyogusa maisha yako. Pia kinatoa mfano wa matukio kuhusu baadhi ya harakati za wananchi waliojitolea kuzilinda haki zao za kikatiba.

Ni mategemeo yetu kuwa msomaji licha tu ya kuburudika, utajifunza na kuishi kwa mujibu wa miongozo ya Kikatiba. Zaidi ya hayo, utawashirikisha na wengine elimu uliyopata katika kijitabu hiki.

**Dr. Helen Kijo Bisimba**
*Mkurugenzi Mtendaji - LHRC*

# Wahusika



**Bonge** - Mpwa wa Anti na Ba'mkubwa



**Anti -** Mke wa Ba'mkubwa




**Ba' mkubwa** - Mkulima




**Mchungaji Boniface** - Kasisi wa kanisa



**Shehe Rashidi** - Shehe wa msikiti


Heh! Mbona mbio hivyo?
Jamani! Kafanyaje kwani?
Kasheshe imetokea hapo sokoni shangazi! Eti wananchi wenye hasira, wamemchoma moto Dalali!


Eti kaiba kiroba cha unga. Nafahamu hakuwa na chochote cha kumlisha dadake mgonjwa.
Mtu akituhumiwa kosa anapewa kifo?!
Si haki!


Jirani, umeyasikia ya Dalali?
Ndiyo. Sikubaliani hata kidogo. Siku hizi kuua kumekuwa kama kukanyaga sisimizi tu?!
Nilishasema, Katiba ilipaswa itulinde.
B


Kwani, Katiba ndo shirika gani vile?
Hata mie sielewi! Nasikia tu 'Katiba, Katiba!'
Si shirika. Ni sheria mama. Sheria zetu zote zinatokea humo.
B



Afadhali viongozi wetu mmepitia hapa. Eti Katiba inawezaje kutulinda?
Aha. Katiba ni makubaliano ya wananchi wenyewe wanavyotaka kujitawala.


Ni maamuzi yetu juu ya namna tunataka nchi yetu ijiendeshe.
Ustaadhi, mbona hayo ni ya wanasiasa?
Sisi tuna katiba pia?


Hapana. Siasa inazaliwa na Katiba. Katiba inaelekeza utendaji wa viongozi wetu.
Aha! Kumbe!
Pia, hutenganisha kazi za Bunge, Mahakama na Serikali.
Sikujua!
B


Leo tumemtenda Mungu pamoja na Dalali mwenyewe dhambi. Haki za Binadamu zimevunjwa.
Alaa, kumbe!
Heh! Ina maana ni kosa letu? Haiwezekani!
B



Ndiyo, Katiba hairuhusu kujichukulia sheria mkononi. Kuna mahakama na polisi
Ndiyo, tunatakiwa tufuate sheria!


Tumekusanyika bila kibali. Si ni makosa?
Katiba inaruhusu kukusanyika na kujumuika kwa jambo halali.


Tumesikia kuna Katiba mpya inaandaliwa. Iliyopo ina matatizo gani?
Mh! Swali zuri. Nitataja machache. Kwanza, haikushirikisha wananchi ilipoandikwa... ...pili, hakuna ulinzi wa haki za binadamu. Zinaweza kubadilishwa wakati wowote.




...tena bado inaruhusu hukumu ya kifo. Wote tuna haki ya kuishi.
Hapana. Tunaweza kuwa na adhabu mbadala.
Si uhalifu ndo utaongezeka?
Hata mimi nina haki ya kuishi!


Wawaa! Leo naelimika hasa!
Pia, Rais ana madaraka makubwa mno. Tena akishinda uchaguzi, hatuwezi kuhoji matokeo yake mahakamani.
Kwa kweli, hiyo si sawa.


Na ardhi yetu je?
Suala la ardhi haijalindwa kikatiba. Hakuna mahali palipotaja masuala ya ardhi katika katiba ya sasa.


Jamani, ina maana katiba ya sasa hivi haina jambo zuri hata moja?
Yamo. Mfano: Asili ya Ujamhuri na kuweka ukomo Rais kuwa madarakani.
Kuna Haki za Binadamu pia, japo hazijitoshelezi



Pia, wanawake tumepewa asilimia 30 za nafasi za uwakilishi.
Wote tuna usawa katika ajira pia


Nani anaandika hiyo Katiba mpya?
wananchi kupitia Tume ya wataalamu na Bunge la Katiba. Si mnakumbuka wataalam walipita kuchukua maoni yetu?
Ooh, tunakumbuka!


Kwa hiyo tunaweza kuchangia maoni yetu, mfano sheria kuhusu wezi?
Ndiyo.


Na pia tunaweza kuchangia maoni kuhusu haki za mfanyabiashara kama mimi?
Na haki za samaki pia?
Ndiyo mama.


Lakini lazima tuangalie baada ya Katiba mpya kama tunatunza haya maoni na haki.
Huyo kijana anaelewa!


Lililotokea leo ni kosa letu wote. Dalali hakuwa na jinsi ya kumsaidia mgonjwa.
Na yule kijana angetuambia tu kuhusu dada yake!
Lakini pia nimesikia watuhumiwa wamekamatwa na polisi.


Ndo maana lazima tupige vita umasikini. Unakuza uhalifu
Si tunaambiwa kipato cha nchi kinaongezeka kila sekunde?
Lakini haionekani kwenye maisha yetu!


Pia kuhubiri tu amani pasipo kugusia uchumi kwa wananchi haitoshi!
Jamani mnataka kuhalalisha uhalifu na mauaji?


Hapana. Hakuna suluhisho bila kung'oa mzizi. Umasikini.
Kuanzia sasa nitaazisha kampeni ya kutengeza fursa kwa vijana kijijini.


Tutaongeza vyuo vya ufundi, shule, miradi ya uzalishaji – mashamba na biashara kwa vijana.
Ndiyo. Tuwape fursa za uongozi pia.


Pia Katiba mpya ihakikishe haki inapatikana katika vyombo vya haki. Wahalifu wasiachiwe hovyo.
R
Hii itaongeza imani yetu kwa vyombo vya usalama.


Baada ya katiba...

# Nini kifanyike:

1. Haki zako zikivunjwa, mweleze kiongozi wa Serikali ya mtaa, washirikishe wanafamilia, marafiki na majirani.
2. Usijichukulie sheria mkononi, tafuta msaada wa sheria.
3. Kuwa tayari kutoa maoni yako na kuchukua hatua wakati wowote.
4. Uwe na uchachu wa mabadiliko katika jamii yako.

